

Kumb Na IPSS/S2065/JI/2021

Jina la Mwanafunzi.....

S.L.P.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPULI KIDATO CHA KWANZA 2021, WILAYA YA TABORA MANISPAA, MKOA WA TABORA.**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 JUMATATU. Unatakiwa kuripoti shuleni saa 1.30 asubuhi.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za Shule**

(a) Sare ya shule hii kwa wanafunzi ni:-

**Wavulana:-**

- suruali upana wa chini kwenye miguu nchi 16 na iwe na marinda mawili (suruali isibane), pia tai inayofanana na suruali. [**Rangi ya kitambaa cha suruali utapewa kipande cha mfano (sampuli)**]
- Shati mbili nyeupe (tetroni) mikono mifupi
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo na visigino virefu
- Soksi nyeusi jozi mbili
- Sweta lenye rangi ya bluu-nyeusi (Dark-blue)
- Mkanda mweusi, usiwe na chuma kikubwa
- Suruali moja rangi nyeusi
- T-shirt rangi ya kijivu isiyo na maandishi yoyote.

**Wasichana:-**

- Sketi iwe ndefu kufika kwenye vifundo vya miguu na marinda yawe nchi mbili, pia tai inayofanana na sketi [**Rangi ya kitambaa cha sketi utapewa kipande cha mfano (Sampuli)**]
- Blauzi mbili nyeupe (tetron) za mikono mifupi
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo na visigino virefu
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili
- Sweta lenye rangi ya bluu-nyeusi (Dark-blue)
- Sketi moja rangi nyeusi ndefu kupita magoti (katikati ya miguu) na marinda yawe nchi mbili.
- T-shirt rangi ya kijivu isiyo na maandishi yoyote.

(b) (**Vazi la Hijabu kwa wanafunzi wa Kiislamu**),

-Juba linalovuka viwiko vya mikono, nusu kanzu nyeupe ya tetroni/mpirampira (isiyobana) na sketi ndefu inayofika kwenye vifundo vya miguu.

**NB:WANAFUNZI WOTE WA KIKE HAWARUHUSIWI KUSUKA NYWELE**

(c) Sare za michezo:-

Wavulana- Bukta rangi ya bluu na T/Shirt rangi ya blue.

Wasichana- Sketi ya rangi ya blue na T/Shirt rangi ya blue.

2.2. Daftari kubwa 12 ( Quire-2), kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu, “Dictionary” na begi jeusi imara la kubebea daftari .

### **3.0.Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii**

3.1.Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
- i) kutunza mali za umma

### **3.2.Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule.**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli. n.k.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kumpa mimba.
- i) Kuoa au kuolewa.
- j)Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m)Kuwa na simu ya mkononi.

### **4.0.Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi.**

- a) Medical Examination Form-ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
- b) Fomu ya mzazi/mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**MUHIMU:** Kulingana na makubaliano ya wazazi na barua yenye Kumb:TMC/ESC/F.1/VOL.II/4 ya tarehe 28/12/2018 inayohusu kibali cha kuchangisha wazazi fedha ya mwalimu wa fizikia na Hisabati,Mzazi unaombwa kuchangia kiasi cha shilingi Elfu sita(6000/Tsh=) kwa muhula au shilingi elfu kumi na mbili(12000/=)kwa mwaka.Mchango huo utapokelewa siku ya kuripoti mwanafunzi.

**Barua ya kibali imebandikwa shuleni kwenye mbao za matangazo.**

.....

MKUU WA SHULE